JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SERA YA TAIFA YA IDADI YA WATU

WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI

2006

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SERA YA TAIFA YA IDADI YA WATU

WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI

2006

YALIYOMO

ORODHA YA AKRONIMI NA VIFUPISHO ii

DIBAJI iii

USULI iv

SURA YA KWANZA 1

1.0 KANUNI 1

1.1 Kanuni za Kuongoza Utekelezaji wa Sera 1

SURA YA PILI 2

2.0 IDADI YA WATU NA MAENDELEO 2

2.1 Mazingira ya Kijamii na Kiuchumi 2

2.2 Ukubwa wa Idadi ya Watu, Vijenzi na Msambao wake 3

2.3 Vijenzi vya Ukuaji wa Idadi ya Watu 3

2.4 Mahusiano ya Idadi ya Watu na Maendeleo 6

2.5 Idadi ya Watu na Jinsia 6

SURA YA TATU 8

3.0 UMUHIMU WA SERA MPYA YA TAIFA YA IDADI YA WATU 8

3.1 Mafanikio, Vipingamizi na Mapungufu 8

3.2 Mambo Mapya na Changamoto Zinazoendelea 10

3.3 Matatizo Makuu kuhusiana na Idadi ya Watu na Maendeleo 11

SURA YA NNE 12

4.0 MALENGO, MADHUMUNI, MASUALA NA MIELEKEO YA SERA 12

4.1 Malengo ya Sera 12

4.2 Ujumuishaji wa Vigeu vya idadi ya watu katika Mipango ya Maendeleo 12

4.3 Ukuaji wa Idadi ya Watu na Ajira 13

4.4 Matatizo ya Makundi Maalumu katika Jamii 14

4.5 Mgaosawa, usawa wa kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake 16

4.6 Afya ya Uzazi 18

4.7 Magonjwa yanayoenezwa kwa Njia ya Ngono, VVU na UKIMWI 20

4.8 Uhifadhi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu 22

4.9 Kilimo, Chakula na Lishe 24

4.10 Umaskini nchini Tanzania 25

4.11 Elimu 26

4.12 Ukusanyaji, Uchakataji, Uhifadhi, Usambazaji wa Data, Mafunzo na Utafiti 27

4.13 Utetezi na Taarifa, Elimu na Mawasiliano 29

SURA YA TANO 30

5.0 MIPANGO YA KIASASI NA DHIMA ZA SEKTA 30

5.1 Mipango ya Kiasasi 30

5.2 Dhima na Majukumu ya Wadau 31

SURA YA SITA 36

6.0 UPANGAJI MIPANGO, UFUATILIAJI NA TATHMINI 36

6.1 Utangulizi 36

6.2 Urazini wa Upangaji Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini 36

6.3 Kiunzi cha Upangaji Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini 36

6.4 Maeneo ya kazi ya kipaumbele ya ufuatiliaji na tathmini 37

6.5 Viashirio vya Ufuatiliaji na Tathmini 37

ORODHA YA AKRONIMI NA VIFUPISHO

AZISE	-	Asasi Zisizo za Serikali
MKUKUTA	-	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
UKIMWI	-	Upungufu wa Kinga Mwilini
VVU	-	Virusi Vya Ukimwi

DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipitisha Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu mwaka 1992. Tangu wakati huo, maendeleo mapya yamekuwa yakitokea kitaifa na kimataifa ambayo yana athari ya moja kwa moja kwenye masuala ya Idadi ya Watu na Maendeleo. Hii imefanya serikali ipitie upya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ili kujumuisha maendeleo hayo mapya. Ndani ya nchi, uchumi umebadilika sana kutoka ule uliokuwa ukipangwa na serikali kuu kuwa uchumi wa soko unaozidi kutawaliwa na sekta binafsi, ambayo ina dhima kubwa katika masuala ya idadi ya watu na maendeleo. Zaidi ya hayo, mnamo Juni 1999, serikali ilizindua dira mpya ya maendeleo, yaani, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Sera hii iliyodurusiwa, yaani Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2006 ina lengo la kuratibu na kuhusisha sera, mikakati na programu nyingine ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya watu na kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake. Itatekelezwa kwa mkabala jumuishi wa sekta mbalimbali kwa upana zaidi. Aidha, Serikali itashirikiana na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), sekta binafsi, jumuiya na mawakala wengine wanaotekeleza sera. Kwa hakika, watu binafsi, vyama vya siasa na makundi mengine katika vyama vya kiraia vinatarajiwa kuwa na dhima ya kuhakikisha kufikiwa kwa malengo na madhumuni ya sera.

Madhumuni makuu ya dira ya maendeleo ya nchi ni kuwaondoa Watanzania kutoka kwenye umaskini na kuinua ubora wa maisha ya watu. Kwa hiyo, Sera inatoa miongozo ya kushughulikia masuala ya idadi ya watu kwa namna jumuishi. Hivyo, inatambua mahusiano baina ya mienendo ya idadi ya watu na ubora wa maisha kwa upande mmoja na ulinzi wa mazingira na maendeleo endelevu kwa upande mwingine. Utekelezaji wake utatoa upeo mpya kwa programu za maendeleo kwa kuhakikisha kwamba masuala ya idadi ya watu yanashughulikiwa kikamilifu.

Ni matumaini yangu kwamba, kwa kuungwa mkono na kwa ushiriki kamilifu wa watu, utekelezaji wa sera hii utafanikiwa.

MHE. JUMA A. NGASONGWA (MB)
WAZIRI
WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI

USULI

Mnamo mwaka 1992, Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu iliyo dhahiri ilikubaliwa rasmi. Kufuatia hatua hiyo, iliandaliwa Programu ya Utekelezaji mnamo mwaka 1995. Kwa kiasi fulani, Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ilijumuisha baadhi ya malengo na madhumuni ya sera na mipango thabiti ya idadi ya watu.

Msisitizo wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ulikuwa ni kutoa kiunzi na miongozo ya kujumuisha vigeu vya idadi ya watu katika mchakato wa maendeleo ili, hatimaye, mienendo ya idadi ya watu iwiane na mienendo mingine ya kijamii na kiuchumi. Hii ni muhimu katika kuharakisha na kufikia maendeleo endelevu na usawa nchini. Vilevile, sera hiyo ilitoa miongozo iliyoamua vipaumbele katika programu ya idadi ya watu na maendeleo. Miongozo hiyo ilibuniwa kuimarisha utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Katika mchakato wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992, kwa kipindi cha miaka kumi, baadhi ya mafanikio yalipatikana na katika baadhi ya maeneo, vipingamizi vilijitokeza. Hata hivyo, maendeleo mapya ambayo yamekuwa yakitokea kitaifa na kimataifa yamelazimisha kudurusiwa kwa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992. Utekelezaji wa Sera mpya ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2006 utafanyika sambamba na Sera ya Idadi ya Watu ya Zanzibar ya mwaka 2003.

SURA YA KWANZA

1.0 KANUNI

1.1 Kanuni za Kuongoza Utekelezaji wa Sera

1.1.1 Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu utaongozwa na kanuni zifuatazo.

i. Kuzingatia madhumuni na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na shabaha zilizowekwa katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia, ambayo miongoni mwa mambo mengine, yanasisitiza dhima ya soko katika kuamua mgao na matumizi ya rasilimali

ii. Kutambua na kuheshimu kaida na mazoea chanya ya kiutamaduni nchini

iii. Kuzingatia usawa na mgaosawa wa kijinsia, haki za watoto na makundi mengine yenye uwezekano wa kuathiriwa kwa urahisi

iv. Uvunaji wekevu wa rasilimali zisizojizalisha za nchi kwa kutilia maanani mahitaji ya vizazi vijavyo na maendeleo endelevu

v. Kutambua na kuthamini dhima kuu ya serikali na ushiriki kamilifu wa AZISE, sekta binafsi, jumuiya na watu binafsi katika masuala ya idadi ya watu na maendeleo

vi. Kuzingatia tofauti za kimkoa na kiwilaya kuhusiana na kiwango cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii pamoja na maumbile ya kidemografia

vii Kutambua ukweli kwamba mtandao wa wadau katika uwanja wa idadi ya watu unaendelea kupanuka na kuthamini dhima yao

viii. Kuunga mkono mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 na sera nyingine zinazoandamana nayo

1.1.2. Sera pia inathibitisha kanuni zifuatazo za Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo uliofanyika mwaka 1994 kama ilivyo katika Mpango wa Kazi.

i. Watu wote wamezaliwa huru na sawa katika heshima na haki. Hivyo, kila mtu ana haki ya maisha, uhuru, usalama, uwajibikaji na heshima.

ii. Watu ni rasilimali muhimu na ya thamani kubwa kwa taifa lolote, na kwa hiyo, watu wote wapewe fursa kutumia uwezo wao wote. Hivyo, watu wote wana haki ya elimu na afya.

iii. Familia ni kitovu cha jamii; hivyo iimarishwe. Vilevile, ina haki ya kupokea ulinzi mpana na msaada.

iv. Wanandoa na watu wote wana haki ya msingi ya kuamua, kwa uhuru na kwa kuwajibika, idadi na mpangilio wa watoto wao na vilevile kupata taarifa, elimu na njia za kufanya hivyo.

v. Kutambua hali ya sekta mbalimbali ya suala la idadi ya watu na haja kubwa ya mkabala wa sekta mbalimbali kutekeleza sera kulingana na masharti

SURA YA PILI

2.0 IDADI YA WATU NA MAENDELEO

2.1 Mazingira ya Kijamii na Kiuchumi

2.1.1 Msisitizo wa Sera ya uchumi ya Tanzania umekuwa ni kudumisha uimara wa uchumi jumla, kwa ukuaji wa uchumi imara, kwa kufuata sera adilifu ya hazina na fedha. Hii imechochea ukuaji wa kuridhisha wa uchumi ambao umesaidiwa na ufanisi katika uuzaji wa bidhaa nje na usimamizi imara wa uchumi. Mafanikio ya kiuchumi pia yanasaidiwa na mazingira mazuri ya kisiasa.

2.1.2 Ukuaji halisi wa Pato la Taifa la Ndani uliofikia wastani wa asilimia 4.5 katika 1996 – 2001 ulipanda hadi asilimia 6.2 mwaka 2002, asilimia 5.7 mwaka 2003, asilimia 6.7 mwaka 2004 na asilimia 6.8 mwaka 2005. Ukuaji huu unatokana na maboresho katika karibu sekta zote za uchumi na vilevile usimamizi imara wa uchumi jumla. Ukuaji wa pato kwa kichwa katika Pato la Ndani ulikuwa hasi katika nusu ya kwanza ya miaka ya 1990; lakini umeongezeka sana na kufikia asilimia 4 kwa miaka ya hivi karibuni. Ongezeko katika ukuaji wa pato kwa kichwa ulikwamishwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa idadi ya watu kilichofikia wastani wa asilimia 2.9 katika kipindi cha kati ya sensa ya mwaka 1988 na 2002.

2.1.3 Tangu mwaka 2002, juhudi za maendeleo nchini Tanzania zinaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo ni tamko la hali ya baadaye inayopendelewa, ambayo taifa inatarajia kufikia na hatua inayowezekana kuchukuliwa ili kuifanikisha. Hii inahitaji uhamasishaji wa watu na rasilimali nyingine katika kufanikisha malengo ya pamoja. Kwa hakika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ilibainisha aina hiyo ya mazingira ya kuwezesha yaliyo muhimu kwa taifa kushamiri kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

2.1.4 Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, kupitia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), unahitaji kuhusishwa kwa sekta za umma na binafsi katika kutekeleza nguzo kuu tatu, yaani, ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, uboreshaji wa maisha ya jamii na ustawi wa jamii na utawala bora na uwajibikaji.

2.2 Ukubwa wa Idadi ya Watu, Vijenzi na Msambao wake

2.2.1 Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 ilionyesha kwamba idadi ya watu Tanzania iliongezeka kutoka milioni 23.1 mnamo 1988 hadi milioni 34.4 mnamo 2002, ikiwa ni wastani wa kiwango cha ukuaji cha asilimia 2.9 kwa mwaka. Sehemu ya watu wenye umri chini ya miaka 15 ilikuwa karibu asilimia 44, wakati wale wenye umri wa miaka 65 na zaidi walikuwa asilimia 4; ikionyesha kwamba Tanzania ina watu wengi vijana. Muundo huu wa kuwepo watu wengi vijana una maana ya ukuaji mkubwa wa idadi ya watu katika siku zijazo, pale vijana wanapoingia katika maisha yao ya uzazi bila kutilia maanani kama uwezo wa kuzaa unapungua au la. Makisio ya idadi ya watu yanaonyesha kwamba Tanzania ina idadi ya watu milioni 37.9 mnamo 2006, na inatarajiwa kufikia milioni 63.5 mwaka 2025.

2.2.2 Sifa muhimu ya maelezo ya idadi ya watu ni msambao wake ndani ya nchi. Uchanganuzi wa msambao wa idadi ya watu kimkoa uliofanywa katika sensa zote zilizopita unaonyesha kuwa karibu theluthi mbili ya watu iko katika robo ya nchi. Kwa mujibu wa Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, msambao wa watu hutofautiana kimkoa ambapo upo kati ya watu 12 kwa kilomita moja ya mraba kwa mkoa wa Lindi, hadi watu 1,700 kwa kilomita moja ya mraba kwa mkoa wa Mjini Magharibi (Zanzibar), na hadi kufikia kiwango cha juu cha watu 1,793 kwa kilometa moja za mraba kwa mkoa wa Dar es Salaam. Sehemu kubwa ya idadi ya watu (asilimia 77 ya Watanzania wote) bado wanaishi vijijini. Hata hivyo, idadi ya watu mijini imekuwa ikikua kwa kasi kwa zaidi ya asilimia 5 kwa mwaka katika miongo mitatu iliyopita. Ukuaji huu wa kasi umesababishwa na uhamaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini kuliko kwa kipengele kingine chochote.

2.3 Vijenzi vya Ukuaji wa Idadi ya Watu

2.3.1 Vijenzi vikuu vya ukuaji wa idadi ya watu katika nchi yoyote ni uzazi, vifo na uhamaji. Nchini Tanzania, uzazi na vifo ni vipengele muhimu sana vinavyoathiri ukuaji wa idadi ya watu katika ngazi ya Taifa. Sensa zilizopita zimeonyesha kwamba kipengele cha uhamaji kimataifa hakijawa na umuhimu. Hata hivyo, kuna maeneo mengine ya Tanzania ambapo uhamaji unaonyesha athari kubwa katika ukuaji wa idadi ya watu, hususani maeneo yanayopokea wakimbizi.

2.3.2 Kiwango cha uzazi nchini Tanzania kinakadiriwa kuwa kimepungua kidogo kutoka watoto 5.8 kwa kila mwanamke wakati wa kipindi cha umri wa kuzaa mnamo mwaka 1996 hadi watoto 5.7 kwa kila mwanamke mnamo mwaka 2004 (*Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania mwaka 2004-05*). Mnamo 2004, Tanzania Bara ilirekodi wastani wa watoto 6.5 kwa kila mwanamke wa maeneo ya vijijini na 3.5 kwa

maeneo ya mijini. Tofauti za wastani huo zenye kuhusiana na viwango vya elimu zinaachana sana. Kiwango cha uzazi kwa wanawake wasio na elimu kilikuwa 6.9, wenye elimu ya msingi ni 5.6 na wenye kiwango cha elimu ya sekondari na elimu ya juu kilikuwa 3.2 (*Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania mwaka 2004-05*). Kwa upande wa Zanzibar, kiwango cha jumla cha uzazi kilishuka kutoka 6.9 mnamo 1996 hadi 5.3 mnamo 2004 (*Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania mwaka 2004-05*).

2.3.3 Kiwango cha juu cha uzazi nchini Tanzania ni matokeo ya sababu kadhaa ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo.

i. Kuolewa mapema na kwa karibu wanawake wote

ii. Umri wa wastani wa ndoa ya kwanza kwa wanawake wenye umri wa miaka 15 – 49 ni miaka 18; na kufikia umri wa miaka 20, zaidi ya asilimia 69 wanakuwa wameolewa walau mara moja (Uchunguzi wa Hali ya Uzazi na Afya ya Mtoto mwaka 1999). Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inataja umri wa chini kabisa kisheria wa ndoa kuwa ni miaka 15 kwa wanawake na miaka 18 kwa wanaume.

iii. Kutokuwepo kanuni madhubuti za uzazi miongoni mwa wanawake wenye umri wa kuzaa:

iv. Kiwango cha kuenea kwa njia za kisasa za kuzuia uzazi kinakadiriwa kuwa asilimia 16 miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 15 – 49 (Uchunguzi wa Hali ya Uzazi na Afya ya Mtoto mwaka 1999).

2.3.4 Vipengele vitano vingine vinachangia katika kiwango kikubwa cha uzazi; navyo vimekitwa katika mfumo wa amali za kijamii na kiutamaduni.

i. Thamani ya mtoto kama chanzo cha nguvukazi majumbani na mashambani na usalama wa kiuchumi na kijamii wa umri mkubwa kwa wazazi

ii. Kupendelea kupata mtoto wa kiume

iii. Hadhi ya chini ya kijamii na kielimu ya wanawake katika jamii inayowazuia kufanya maamuzi kuhusu uzazi na matumizi ya huduma za uzazi wa mpango

iv. Tofauti kubwa za umri baina ya wanandoa zinazokwamisha mawasiliano kuhusu masuala yanayohusiana na afya ya uzazi

v. Dhima za kijamii, kiuchumi na kijinsia

2.3.5 Kiwango cha vifo kimepungua sana nchini Tanzania katika miongo kadhaa. Vipengele vikuu vinavyochangia katika kupungua huku ni upatikanaji wa huduma bora za afya pamoja na usafi wa mazingira. Kiwango cha vifo kinakadiriwa kuwa kimepungua kutoka vifo 22 kwa kila watu 1,000 mnamo 1967 hadi vifo 15 mnamo mwaka 1988, na kuongezeka kidogo hadi 16 mnamo mwaka 2002. Kiwango cha vifo vya watoto wachanga kwa watoto 1,000 waliozaliwa hai inakadiriwa kushuka kutoka 170 mnamo 1967, hadi 115 mnamo 1988, na kisha hadi vifo 95 mnamo 2002. Huko Zanzibar, kiwango cha vifo vya watoto wachanga ni vifo 82 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Katika kipindi hicho, kiwango cha vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai kilipungua kutoka 260 mnamo 1967, 191 mnamo 1988 hadi 153 mnamo 2002. Kiwango cha vifo kinachopungua kinaakisiwa katika viwango vya muda wa kuishi vinavyoongezeka wakati wa kuzaliwa kutoka kiwango cha karibu miaka 40 mnamo 1967 hadi karibu miaka 50 mnamo 1988, na kilikadiriwa kuwa karibu miaka 51 mnamo 2002. Pamoja na kupungua huku, kiwango cha vifo bado ni cha juu kwa viwango vya dunia. Kiwango cha vifo vya uzazi vya akina mama si cha juu tu, bali kinaendelea kuwa tatizo kubwa nchini, kwani kiwango hicho kimeongezeka kutoka vifo 529 kwa kila wanawake 100,000 mnamo 1996 (*Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania mwaka 1996*) hadi 578 kwa kila wanawake 100,000 mnamo 2004 – 05 (*Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania mwaka 2004-05*).

2.3.6 Uhamaji wa kutoka vijijini kwenda mijini umekuwa aina kuu ya uhamaji nchini Tanzania kwa miaka mingi. Kuongezeka kwa uhamaji kutoka vijijini kwenda mijini kumesababisha ongezeko la kiwango cha ukuaji miji, hususani katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Arusha na Zanzibar. Sehemu ya idadi ya watu inayoishi katika maeneo ya mijini imeongezeka kutoka asilimia 5 mnamo mwaka 1967 hadi asilimia 13 mnamo mwaka 1978; na kutoka asilimia 21 mnamo mwaka 1988 hadi asilimia 27 mnamo mwaka 2002. Kati ya miaka 1978 na 1988, idadi ya wakazi wa mijini nchini Tanzania iliongezeka kwa asilimia 53. Kuna tofauti baina ya mikoa kuhusiana na kiwango cha ukuaji miji: Dar es Salaam peke yake ilikuwa na karibu asilimia 25 ya jumla ya wakazi wa mijini mnamo mwaka 1988. Kiwango cha uhamaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini ambacho kilikuwa hakijawahi kutokea kimeongeza mzigo kwa huduma za umma na miundombinu ya kijamii ambazo tayari zimeishaelemewa. Uhamaji wa kutoka vijijini kwenda mijini pia umechangia katika tofauti kwa ngazi za mkoa na wilaya kutokana na shinikizo la idadi ya watu kwenye rasilimali. Tofauti hizo zinaweza kuonekana kwa urahisi katika tofauti za msongamano wa watu kati ya wilaya, kata na vijiji.

2.4 Mahusiano ya Idadi ya Watu na Maendeleo

2.4.1 Kuna uhusiano wa karibu kati ya ukuaji wa idadi ya watu na maendeleo. Katika muda mfupi, athari za ukuaji wa idadi ya watu zinaweza kuonekana kuwa ndogo. Lakini zinaanzisha mchakato limbikizi, ambao athari yake hasi kwenye sura mbalimbali za maendeleo zinaweza zikawa muhimu sana katika muda wa kati na mrefu. Hii ni kwa sababu vigeu vya idadi ya watu vinaathiri maendeleo na ustawi wa mtu mmoja mmoja, familia, jumuiya katika ngazi ndogo na katika ngazi ya wilaya, mkoa na taifa zima katika ngazi ya jumla. Athari na miitikio ya shinikizo la idadi ya watu zinahusiana katika ngazi zote.

2.4.2 Ukuaji wa kasi wa idadi ya watu katika mazingira ya ukuaji mdogo kiuchumi huelekea kuongeza matumizi, ukiwa unaondoa rasilimali kutoka kwenye akiba ya vitegauchumi vya uzalishaji; na hivyo kuelekea kupunguza kasi ya ukuaji wa uzalishaji wa taifa kupitia uundwaji mdogo wa mtaji. Matatizo yanayosababishwa na ukuaji wa kasi wa idadi ya watu yana athari kubwa na yenye kuonekana katika bajeti za umma kwa ajili ya afya, elimu na sekta nyingine za maendeleo ya rasilimali watu.

2.4.3 Idadi ya watu na maendeleo yanaathiriana. Athari inaweza ikawa chanya au hasi kutegemea vipengele na hali nyingine. Kwa upande wa Tanzania, vipengele vilivyotajwa awali vya demografia vinaingiliana na kusababisha matatizo yafuatayo walau katika muda mfupi.

i. Ukuaji haraka wa idadi ya vijana unahitaji ongezeko la matumizi yaliyolengwa kwenye huduma za kijamii kama vile elimu, afya, maji na makazi.

ii. Ukuaji wa haraka wa nguvukazi unahitaji uwekezaji mkubwa katika maendeleo ya rasilimali watu, na vilevile mikakati ya maendeleo inayohakikisha fursa za uundaji wa ajira katika siku zijazo.

iii. Ukuaji wa haraka wa idadi ya watu katika muktadha wa kuondoa umaskini hupunguza uwezekano wa kufikia ukuaji endelevu wa uchumi.

2.5 Idadi ya Watu na Jinsia

2.5.1 Sura za kijinsia za kaya na idadi ya watu kwa ujumla zina athari kubwa kwenye sehemu nyingi za maendeleo ikiwa ni pamoja na afya, elimu, umaskini, n.k.

2.5.2 Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 ilionyesha kuwa wanaume wamefanikiwa zaidi kupata elimu kuliko wanawake. Wakati kiwango cha taifa cha kujua kusoma na kuandika kilionekana kuwa asilimia 77, hii pia ni wastani wa kitaifa wa kiwango cha kujua kusoma na kuandika kwa wanaume, wakati kwa wanawake ni asilimia 65.

2.5.3 Sehemu kubwa ya kaya (hadi kufikia asilimia 32.7 ya kaya zote) zilikuwa na wakuu wa kaya wanawake. Katika maeneo ya vijijini ni asilimia 32.4 ya kaya ziliongozwa na wanawake; na katika maeneo ya mijini ni asilimia 33.6. Kimkoa, Mwanza ilikuwa na sehemu kubwa ya kaya zinazoongozwa na wanawake (asilimia 45), ikifuatiwa na Iringa (asilimia 42) wakati Ruvuma, yenye asilimia 24, ikiwa ya chini kabisa. Ikiwekwa kwa namna tofauti kidogo, kwa kila kaya 100 zilizoongozwa na wanaume nchini Tanzania mnamo 2002, kulikuwa na kaya 49 zilizoongozwa na wanawake. Katika maeneo ya vijijini, kwa kila kaya 100 zinazoongozwa na wanaume kuna kaya 48 zinazoongozwa na wanawake, wakati kwa maeneo ya mijini kuna uwiano wa kaya 51 zinazoongozwa na wanawake kwa kila kaya 100 zinazoongozwa na wanaume. Ripoti ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 pia imeonyesha kuwa sehemu fulani ya kaya (ndogo iwavyo) zinaongozwa na watoto; hii ikiwa ni athari ya janga la VVU na UKIMWI.

2.5.4 Hadhi ya ndoa pia huelekea kuwa na athari (moja kwa moja au kwa namna isiyo ya moja kwa moja) kwa hali nyingi za ustawi wa kijamii na kiuchumi za wanawake na wanaume. Hadhi ya ndoa huathiri uzazi, matumizi ya vifaa vya uzazi wa mpango, n.k. Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, imeonyesha kwamba asilimia 24 ya jumla ya wanawake walikuwa wameolewa wakati wanaume waliooa walikuwa asilimia 21 ya jumla yao. Vilevile wanawake huolewa katika umri wa mapema kuliko wanaume. Wakati umri wa wastani wa nchi katika ndoa ya kwanza ni miaka 23.3, ule wa wanaume ni miaka 25.8 wakati kwa wanawake ni miaka 21.1. Katika maeneo ya vijijini, wanaume na wanawake huoa na kuolewa mapema zaidi kuliko umri wa wastani wa Taifa wa ndoa ya kwanza. Lakini katika maeneo ya mijini, hali ni kinyume. Watu huoa na kuolewa katika umri wa baadaye kuliko wenzao wa vijijini. Umri wa wastani wa ndoa ya kwanza mijini ni wa juu kuliko wastani wa kitaifa: kwa wanaume ikiwa ni miaka 28, na kwa wanawake miaka 23.3.

Hata hivyo, unapotumia kipimo cha jumla cha ustawi, yaani, muda anaotarajiwa mtu kuishi wakati wa kuzaliwa, Sensa ya mwaka 2002 imeonyesha kwamba wanawake wanawazidi kidogo muda wa kuishi wanaume: wakiwa wanaishi miaka 52 wakati wanaume wanaishi miaka 51.

SURA YA TATU

3.0 UMUHIMU WA SERA MPYA YA TAIFA YA IDADI YA WATU

Malengo na madhumuni ya Sera mpya ya Taifa ya Idadi ya Watu ni kutoa kiunzi na miongozo kwa ujumuishaji wa vigeu vya idadi ya watu katika mchakato wa maendeleo. Sera hiyo inatoa miongozo inayoamua vipaumbele katika programu za idadi ya watu na maendeleo; na vilevile kuimarisha utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Tanzania iliikubali Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu dhahiri mnamo mwaka 1992 na yafuatayo ni mafanikio, vipingamizi na mapungufu yake.

3.1 Mafanikio, Vipingamizi na Mapungufu

3.1.1 Mafanikio

Mafanikio ya sera dhahiri na thabiti zilizopita za idadi ya watu ni pamoja na yafuatayo.

Kuongezeka kwa mwamko wa masuala ya idadi ya watu

i. Uzazi, vifo vya watoto wachanga na watoto vimepungua kwa muda; wakati wastani wa muda anaotarajiwa mtu kuishi wakati wa kuzaliwa umekuwa ukipanda.

ii. Mwamko kuhusu VVU na UKIMWI umefikia zaidi ya asilimia 95 miongoni mwa wanaume na wanawake wenye umri wa zaidi ya miaka 15.

iii. Mwamko zaidi wa uhusiano na mahusiano kati ya idadi ya watu, rasilimali, mazingira na maendeleo katika ngazi zote

iv. Kupanuka na/au kuanzishwa kwa mafunzo ya idadi ya watu katika asasi za elimu ya juu nchini

v. Idadi na uwezo ulioongezeka wa AZISE na mashirika ya dini yanayojihusisha na shughuli zinazohusiana na idadi ya watu ikiwa ni pamoja na utetezi, uhamasishaji wa jamii, utoaji wa huduma na kujenga uwezo

vi. Kiwango cha kuenea kwa njia za kisasa za uzazi wa mpango kiliongezeka kutoka karibu asilimia 18.4 mnamo 1996 hadi asilimia 26 mnamo 2004 (*Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania 2004 – 2005*) kutokana na maarifa zaidi.

vii. Kuongezeka kuhusishwa na kuungwa mkono sera na watunga sheria kuhusu masuala ya idadi ya watu kupitia uundwaji na utendaji wa Chama cha Wabunge wa Tanzania cha Idadi ya Watu na Maendeleo, Kundi la Wabunge linalojihusisha na VVU na UKIMWI, Mawaziri Wanawake na Wabunge wa Afrika (Kitengo cha Tanzania)

viii. Ujumuishwaji wa Elimu ya Maisha ya Familia katika mitaala ya shule za sekondari na Vyuo vya Ualimu

ix. Ujumuishwaji wa elimu ya VVU na UKIMWI katika mitaala ya shule za msingi na sekondari na Vyuo vya Ualimu

x. Kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi na kuikubali Sera ya Taifa kuhusu VVU na UKIMWI

xi. Kubuni na kutekeleza Kiunzi cha Taifa cha Mikakati ya Sekta Mbalimbali na Mkakati wa Sekta ya Afya kwa VVU na UKIMWI 2003 -2007

xii. Kubuni Miongozo ya Sera ya Taifa kuhusu Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

xiii. Mpango wa Kazi wa Taifa 2001-2025 wa kuharakisha usitishaji wa Ukeketaji na mazoea ya kijadi yenye madhara

xiv. Kuongeza mgao wa rasilimali kwa utafiti, mafunzo na ukusanyaji wa data

xv. Mkakati wa Afya ya Uzazi kwa Vijana wadogo

xvi. Kuandaa programu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu, uhamasishaji wa rasilimali za ndani na nje kwa utekelezaji wa programu za idadi ya watu

xvii. Kubuni Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake

xviii. Kiunzi kilichoboreshwa kwa utekelezaji wa uingizaji wa masuala ya jinsia katika sekta mbalimbali

3.1.2 Vipingamizi na mapungufu

Vipingamizi na mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 na sera thabiti ya idadi ya watu ni pamoja na yafuatayo.

i. Rasilimali watu yenye mafunzo isiyotosheleza katika ngazi zote za utekelezaji

ii. Rasilimali zisizotosheleza za fedha na vifaa

iii. Kutotosheleza kwa data zenye kuhusiana na umri na idadi ya watu zilizotenganishwa kijinsia

iv. Kutoanzishwa kwa uratibu wa sera iliyopangwa na mipango ya utekelezaji

v. Sera ambazo, kwa kiasi kikubwa, hushughulikia shughuli za uzazi wa mpango na mpangilio wa watoto ziliathiri ushiriki mdogo wa wahusika katika masuala mengine ya afya ya uzazi

vi. Kuweka msisitizo zaidi kwenye kufikia shabaha za kidemografia badala ya mahitaji ya watu binafsi (wake kwa waume)

vii. Utambuzi usioridhisha wa uhusiano baina ya umaskini, idadi ya watu, mazingira, jinsia na maendeleo

viii. Utetezi usioridhisha wa kuhakikisha kuungwa mkono kunakohitajika katika masuala ya idadi ya watu na maendeleo

ix. Uwezo na rasilimali zisizotosheleza za AZISE zinazojihusisha na shughuli zenye kuhusiana na idadi ya watu

3.2 Mambo Mapya na Changamoto Zinazoendelea

3.2.1 Tangu kukubaliwa kwa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu mwaka 1992, kumekuwepo na maendeleo mapya yanayotokana na maendeleo yaliyojitokeza kitaifa na kimataifa. Hizi ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Dira ya Maendeleo Zanzibar 2020, Mkakati wa Kupunguza Umaskini, Marekebisho ya Kisekta, Elimu ya Msingi kwa Watoto Wote 2001, Sera ya Maendeleo Vijijini, Mkakati wa Maendeleo Vijijini, na Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Umaskini. Kimataifa, maendeleo mapya ni haya yafuatayo.

i. Mkutano wa Mazingira na Maendeleo wa Rio 1992
ii. Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo wa Cairo 1994
iii. Mkutano wa Nne wa Dunia wa Wanawake, 1995
iv. Mkutano Mkuu wa Dunia wa Maendeleo ya Jamii, Copenhagen 1995
v. Mkutano Mkuu wa Jiji la Istanbul 1996
vi. Mkutano wa Dunia wa Chakula 1997
vii. Kuanzishwa na kukubaliwa kwa Malengo ya Maendeleo ya Milenia
viii. Mkutano Mkuu Maalumu wa Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu VVU na UKIMWI 2001
ix. Mkutano Mkuu wa Dunia wa Maendeleo Endelevu 2002

3.2.2 Maendeleo mapya yaliyotajwa hapo juu yameibua mabadiliko katika mikabala na mielekeo ya sera ili kushughulikia masuala haya tisa yafuatayo.

i Masuala ya idadi ya watu kiujumla zaidi katika mipango ya maendeleo na vilevile kutambua dhima za washirika wengine - vyama vya kiraia, AZISE na sekta binafsi
ii. Ushiriki wa vyama vya kiraia, AZISE na sekta binafsi
iii. Umasikini katika maana yake pana, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na usawa katika matumizi na mgawo wa rasilimali kati ya wanawake na wanaume na/au makundi mengine mbalimbali ya kijamii
iv. Sheria za kibaguzi na mazoea ya kijadi yenye madhara dhidi ya wanawake na wanaume
v. Masuala yanayohusiana na afya ya uzazi na haki za uzazi
vi. Mahusiano kati ya idadi ya watu na maendeleo endelevu
vii. Mahitaji ya msingi ya makundi mbalimbali katika jamii
viii. Matatizo ya makosa ya jinai, umaskini, ukosefu wa ajira, miundombinu duni, n.k. yanayohusiana na viwango vya ukuaji miji
ix. Janga la VVU na UKIMWI kwa mtazamo wa sekta mbalimbali na serikali kuhamasisha rasilimali

3.2.3 Changamoto nyingine ambazo zimeibua haja ya kupitiwa kwa sera ni pamoja na hizi zifuatazo.

i. Aina na viwango vilivyoongezeka vya vurugu zenye misingi ya kijinsia, mazoea ya kijadi yenye madhara ikiwa ni pamoja na ukeketaji, dhuluma za kijinsi, kuacha na kutelekeza watoto
ii. Haja ya elimu inayotakiwa bora na nafuu na mafunzo katika ngazi zote
iii. Kuenea sana kwa magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya Ngono, VVU na UKIMWI
iv. Viwango vya juu vya mimba kwa vijana wadogo na kuzaa mapema kwenye umri mdogo
v. Mimba na uzazi wa mara kwa mara
vi. Ukosefu wa ajira unaoongezeka kutokana na utendaji duni wa kiuchumi ukiwa sambamba na ongezeko kubwa la nguvukazi
vii. Vifo vinavyoendelea vya uzazi vya akinamama, watoto wachanga na watoto
viii. Ukuaji wa haraka na usiopangwa wa miji
ix. Hadhi ya chini wanayopewa wanawake katika jamii
x. Programu zisizoridhisha za kushughulikia mahitaji mahsusi ya afya ya uzazi ya makundi mahsusi ya watu
xi. Matukio yaliyoongezeka ya matumizi ya madawa ya kulevya
xii. Mahitaji yanayoongezeka ya makundi yenye matatizo, ikiwa ni pamoja na yatima

3.3 Matatizo Makuu kuhusiana na Idadi ya Watu na Maendeleo

3.3.1 Matatizo makuu ya sera ya idadi ya watu yanajumuisha maeneo yafuatayo: masuala ya idadi ya watu na mipango ya maendeleo; usawa, mgaosawa, na haki ya kijamii; afya ya uzazi; maliasili; uzalishaji chakula; taarifa na kanzi ya data na utetezi. Kwa kuzingatia haya, kuna haja ya kufanya yafuatayo.

i. Kuhamasisha na kugawa rasilimali zaidi kwa miundombinu, kujua kusoma na kuandika, huduma za afya na elimu, kwa lengo la kuongeza ubora, ufikikaji na upatikanaji
ii. Kutumia kikamilifu na kiuendelevu maliasili na mazingira ili kupanua uchumi
iii. Kupanua uzalishaji wa kilimo kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya chakula na lishe
iv. Kuhakikisha upatikanaji wa wakati na mpana wa data zilizotenganishwa za jinsia, na taarifa ya upangaji mipango razini na madhubuti, na vilevile kwa ubunifu na utekelezaji wa programu katika ngazi zote
v. Kuingiza jinsia katika mipango na programu za maendeleo
vi. Kubuni programu zinazoongeza ushiriki kamilifu wa makundi maalumu katika jamii
vii. Kuingiza masuala ya VVU na UKIMWI katika mipango ya idadi ya watu na maendeleo
viii. Kugawa rasilimali na kutayarisha vifaa vya Taarifa, Elimu na Mawasiliano kwa ajili ya utetezi

SURA YA NNE

4.0 MALENGO, MADHUMUNI, MASUALA NA MIELEKEO YA SERA

4.1 Malengo ya Sera

Lengo kuu la Sera ya idadi ya watu ni kuiwezesha Tanzania kufikia kiwango cha maisha kilichoboreshwa na kufanikisha ubora wa maisha ya watu wake. Vipengele muhimu vya ubora wa maisha ni pamoja na afya na elimu bora; chakula cha kutosha na makazi bora mazingira imara; mgaosawa; ubora wa kijinsia, na usalama wa watu binafsi. Aidha, Sera ina lengo la kuelekeza ubunifu wa Sera za Kisekta, na mikakati na mipango mingine inayohakikisha maendeleo ya watu. Malengo mahsusi ya sera hii ni kufanikisha yafuatayo.

i. Maendeleo endelevu na kuondoa umaskini
ii. Kuongeza na kuboresha upatikanaji na ufikiaji wa huduma bora za kijamii
iii. Kuwa na mgaosawa, usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa wanawake, haki ya kijamii na maendeleo kwa watu wote
iv. Mpangilio mzuri baina ya idadi ya watu, matumizi ya rasilimali na mazingira

Kwa msingi wa matatizo yaliyoelezwa katika Sura ya Tatu, mambo yanayotazamwa katika sehemu 4.2 – 4.13 hapa chini yamebainishwa kama maeneo ya kipaumbele yatakayoshughulikiwa na sera hii.

4.2 Ujumuishaji wa Vigeu vya idadi ya watu katika Mipango ya Maendeleo

4.2.1 Masuala

Ujumuishaji wa vigeu vya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na sera bado haujatambuliwa kikamilifu. Hii ni kutokana na vipengele kadhaa ikiwa ni pamoja na yafuatayo.

i. Utambuzi usioridhisha wa uhusiano baina ya vigeu vya idadi ya watu na maendeleo
ii. Uwezo mdogo katika ngazi za kitaifa, kisekta na kiwilaya wa ujumuishaji thabiti wa vigeu vya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo
iii. Kutotosheleza kwa data za kijinsia zilizotenganishwa za sasa na jumuishi
iv. Kutotambuliwa, na hivyo, kutoongozwa kwa uhusishaji wa sekta binafsi, jumuiya na kaya za sehemu husika katika mambo yanayofungamana na idadi ya watu na maendeleo

4.2.2 Madhumuni ya Sera

i. Kuwianisha idadi ya watu na ukuaji wa uchumi
ii. Kukuza uzalishaji wa data za kijinsia zilizotenganishwa
iii. Kuhamasisha rasilimali zinazohitajika kwa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu
iv. Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na watu katika juhudi za maendeleo
v. Kukuza raghba ya kisiasa na kujifunganisha na masuala ya idadi ya watu na maendeleo

4.2.3 Mwelekeo wa Sera

i. Kuongeza mwamko kwa viongozi na jumuiya kuhusu uhusiano kati ya idadi ya watu, rasilimali, mazingira, kuondoa umaskini, na maendeleo endelevu
ii. Kujenga uwezo wa wapangaji mipango katika ngazi zote kuingiza masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo kwa mtazamo wa kijinsia
iii. Kuhamasisha sekta binafsi na jumuiya ya sehemu husika kujihusisha kimatendo katika kuanzisha, kutekeleza na kugharimia programu za idadi ya watu
iv. Kuimarisha juhudi katika ukusanyaji, uchakataji, uchanganuzi na usambazaji wa data za kijinsia zilizotenganishwa
v. Kukuza na kuimarisha vyanzo vingine vya data na taarifa za idadi ya watu

4.3 Ukuaji wa Idadi ya Watu na Ajira

4.3.1 Masuala

Nguvukazi ya Tanzania inafafanuliwa kama watu wenye kujishughulisha kiuchumi wa umri wa miaka 10 hadi 64. Matokeo ya Utafiti wa Nguvukazi Jumuishi wa 2000/1 yanaashiria kwamba nguvukazi inayojishughulisha ni milioni 17.8. Makisio yanaonyesha kwamba kati ya watu 659,000 na 750,000 wamekuwa wakiingia katika nguvukazi kila mwaka. Uchanganuzi wa ajira unaonyesha kwamba sekta ya kilimo, sekta isiyo rasmi na sekta binafsi rasmi zinaajiri watu zaidi. Kwa kipindi kirefu kinachokuja, sekta ya kilimo itaendelea kuwa mwajiri mkubwa ukilinganisha na sekta nyingine. Watu wasioajiriwa kwa kipindi hicho walikuwa milioni 2.3, na karibu nusu yao walikuwa wakiishi katika maeneo ya mijini. Ukosefu wa ajira kwa jiji la Dar es Salaam peke yake ulikuwa asilimia 46.5, wakati katika maeneo mengine ya mijini ulikuwa asilimia 25.5; na katika maeneo ya vijijini ulikuwa asilimia 8.4.

Matokeo ya utafiti yamedhihirisha pia kwamba ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa miongoni mwa vijana. Vijana wa kike wana uwezekano wa kukumbwa kwa urahisi zaidi na tatizo hili kuliko wa kiume.

4.3.2 Madhumuni ya Sera

Kuunda mazingira mazuri kwa ajili ya kuongezeka kwa fursa za ajira katika maeneo ya vijijini na mijini

4.3.3 Mwelekeo wa Sera

i. Kuunda mazingira yenye kuwezesha kwa ajili ya uwekezaji katika sekta zote, hususani katika maeneo ya vijijini
ii. Kukuza fursa za kujiajiri katika sekta isiyo rasmi
iii. Kutoa taarifa za soko la ajira kwa waajiri na kwa watafuta ajira
iv. Kukuza muundo endelevu wa kifamilia
v. Kukuza utekelezaji wa Shughuli za Biashara Ndogo na za Kati katika maeneo ya vijijini

4.4 Matatizo ya Makundi Maalumu katika Jamii

4.4.1 Masuala

Watoto, vijana, wazee na watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi katika jamii yanayohitaji programu maalumu ya kuwezesha ushiriki wao kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Wakimbizi, kama kundi jingine maalumu katika jamii, wanahitaji uangalifu maalumu na hatua za kuziwahi athari zozote hasi nchini.

Watoto

Katika sera hii, watoto wanafafanuliwa kama wale walio na umri wa chini ya miaka 15. Kundi hili ni asilimia 44.24 ya watu wa Tanzania (Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya 2002)

i. Mazoea ya kiutamaduni yaliyopitwa na wakati na kuvunjika kwa familia na kaida za jamii vimewafanya watoto wakabiliane na matatizo kama vile utapiamlo, ajira ya watoto, kutupwa, ukahaba na kudhulumiwa kijinsi.
ii. Aidha, janga la VVU na UKIMWI limesababisha ongezeko la idadi ya watoto yatima na watoto wa mitaani.

Vijana

Katika sera hii, vijana wanafafanuliwa kama wale wenye umri wa kati ya miaka 15 – 24 Hili kundi ni asilimia 19.58 ya watu wa Tanzania (Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya 2002)

i. Tija na uzalishaji mdogo, upungufu wa mahitaji ya msingi na ukosefu wa ajira na huduma za kisasa katika maeneo ya vijijini vimewalazimisha vijana kuhamia mijini kwa matumaini ya kukidhi matarajio yao lakini wengi wao wameishia kukatishwa tamaa wanaposhindwa kuyapata.

ii. Hiki ndicho kikundi chenye uwezekano wa kukumbwa kwa urahisi zaidi na janga la VVU na UKIMWI.

Wazee

Kwa mujibu wa Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya 2002, wazee wenye umri wa miaka 65 na zaidi walikuwa asilimia 4 ya watu wa Tanzania. Tatizo linalowakabili wazee wengi ni pamoja na upweke, mapato ya chini, kupungua kwa heshima kwao na kutopatikana kwa huduma za afya; na katika maeneo mengine wanasumbuliwa kwa misingi ya imani za kichawi.

Watu wenye ulemavu

Sehemu ya watu wenye ulemavu wa kimwili na wa kiakili ni asilimia 8 (Sensa ya 2002). Miongoni mwa matatizo yanayowakabili watu hawa ni pamoja na unyanyapaa, ubaguzi na ukosefu wa mafunzo, ajira na vifaa vya kusaidia kama vile baiskeli za walemavu, vitabu kwa ajili ya vipofu, magongo ya kutembelea na viungo bandia.

Wakimbizi

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 1960, Tanzania imekuwa mwenyeji wa idadi kubwa ya wakimbizi kutoka nchi nyingine za Kiafrika. Idadi kubwa ya wakimbizi iliingia nchini mnamo mwaka 1994 kufuatia mapigano ya kiraia katika baadhi ya nchi za Maziwa Makuu. Miongoni mwa matatizo yanayohusiana na wakimbizi ni ukataji misitu, ongezeko la makosa ya jinai, kutokea kwa magonjwa ya milipuko na kuzorota kwa huduma za kijamii na usalama wa ndani.

4.4.2 Madhumuni ya Sera

i. Kuongeza malezi sahihi kwa watoto na vijana

ii. Kuwawezesha vijana kupata rasilimali

iii. Kukuza ushiriki wa vijana katika ufanyaji maamuzi

iv. Kukuza ustawi wa wazee wenye ulemavu na makundi mengine yote yenye matatizo

v. Kutetea kujihusisha kwa jumuiya ya kimataifa kushughulikia matatizo ya wakimbizi na watu walioondolewa makwao

4.4.3 Mwelekeo wa Sera

Watoto

i. Kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika juhudi za maendeleo ya watoto
ii. Kukuza haki za watoto
iii. Kukuza ubia na programu zenye kulengwa kwa yatima na watoto wa mitaani

Vijana

i. Kukuza ushiriki wa vijana katika ufanyaji maamuzi na kuratibu programu za maendeleo kwa vijana kujitegemea na kupata rasilimali
ii. Kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika juhudi za maendeleo ya vijana
iii. Kukuza haki za vijana

Wazee

i. Kuhimiza sekta binafsi, AZISE na mashirika ya kidini kuwekeza katika utoaji wa huduma za kijamii, hususani huduma za afya kwa wazee
ii. Kuanzisha hatua za usalama wa kijamii zinazoshughulikia matatizo ya wazee
iii. Kuhimiza mitandao ya misaada ya kijadi iliyokitwa katika jumuiya kwa wazee
iv. Kutetea uanzishwaji wa shughuli za kuzalisha mapato kwa wazee

Watu wenye ulemavu

i. Kuhimiza sekta binafsi, AZISE na mashirika ya kidini kuwekeza katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa watu wenye ulemavu
ii. Kuongeza ubunifu wa stadi na upatikanaji wa fursa kwa watu wenye ulemavu
iii. Kuanzisha hatua za usalama wa kijamii zinazoshughulikia matatizo ya watu wenye ulemavu

Wakimbizi

i. Kutetea kuhusika kwa jumuiya ya kimataifa kushughulikia matatizo ya wakimbizi

4.5 Mgaosawa, usawa wa kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake

4.5.1 Jinsia inahusu dhima na majukumu yaliyoundwa kijamii ya wanawake na wanaume katika utamaduni au mahali fulani. Dhima hizo zinaathiriwa na mtazamo na matarajio yanayotokana na vipengele vya kiutamaduni, kisiasa, kimazingira, kiuchumi, kijamii na kidini; na vilevile mapendeleo ya kidesturi, kisheria, kitabaka na kibinafsi au kiasasi.

Mgaosawa kijinsia ni haki katika kugawa manufaa na majukumu. Ni fursa sawa, kutendewa sawa mbele ya sheria na ufikiaji na udhibiti sawa wa rasilimali na huduma za jamii. Usawa kijinsia ni kugawana madaraka miongoni mwa wanawake na wanaume, si katika kiwango cha mtu binafsi, bali kimsingi, katika ngazi ya kiasasi. Inataka kuwepo kwa haki, majukumu na wajibu sawa na si kufanana.

4.5.2 Masuala

Dhima za kijinsia za kijadi zilizozoeleka zinawakinza wasichana na wanawake kupata fursa.

i. Dhima za wanawake za kiuchumi, kijamii na kinyumbani zinahusu zaidi kuzaa watoto; hali inayohatarisha afya zao.
ii. Mimba za utotoni na kuzaa miongoni mwa wasichana wadogo huwa kunazuia mafanikio yao ya kielimu, upatikanaji wa stadi na matarajio ya kazi.
iii. Muundo wa kijamii wa jamii unaongeza mzigo wa kazi kwa wanawake.
iv. Ushiriki na mchango wa wanawake katika maendeleo vimekwamishwa na mazoea ya kibaguzi. Wanawake wana uwezo mdogo wa kupata na kudhibiti mali na urithi; na vilevile ushiriki katika elimu rasmi na sekta za ajira.
v. Ukeketaji, vurugu zenye misingi ya kijinsia na dhuluma za kijinsi ni vikwazo dhidi ya maendeleo ya kijamii.

4.5.3 Madhumuni ya Sera

i. Kukuza mgaosawa, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika ngazi zote
ii. Kubadilisha amali za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na mitazamo inayokwamisha usawa na mgaosawa kijinsia

4.5.4 Mwelekeo wa Sera

i. Kuongeza mwamko wa jamii juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wote
ii. Kukuza ushiriki wa wanawake katika ufanyaji maamuzi, ikiwa ni pamoja na mambo ya kisiasa katika ngazi zote
iii. Kukuza fursa za ajira kwa wanawake na usalama wa ajira
iv. Kuondoa aina zote za ubaguzi na vurugu zenye misingi ya kijinsia
v. Kuunda mazingira mazuri ya kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake
vi. Kuhakikisha uingizwaji wa masuala ya wanawake katika mipango na sera za maendeleo
vii. Kuunda mazingira mazuri kwa wadau mbalimbali kuendesha shughuli za utetezi kuhusu masuala ya jinsia na idadi ya watu

4.6 Afya ya Uzazi

4.6.1 Afya ya uzazi ni hali ya ustawi kamili kimwili, kiakili na kijamii, na si tu hali ya kutokuwepo maradhi au udhaifu, katika mambo yote yanayohusu mfumo wa uzazi ikiwa ni pamoja na kazi na michakato yake. Hii ina maana ya haki ya kuwa na maisha ya ngono ya kuridhisha na salama, uwezo wa kuzaa salama na uhuru wa kuamua lini na mara ngapi ufanye hivyo. Afya ya uzazi na mtoto nchini Tanzania inajumuisha mambo yafuatayo: huduma za ujauzito, huduma za wakati wa kujifungua, huduma za dharura za uzazi, huduma za mtoto mchanga, huduma za baada ya kujifungua, huduma za baada ya kutoa mimba, uzazi wa mpango; kinga na usimamizi wa magonjwa yanayosambazwa kwa njia ya ngono, VVU na UKIMWI, saratani, magonjwa ya utotoni, magonjwa yanayochanjwa; lishe, na vilevile kinga na usimamizi wa fistula na maradhi mengine yanayotokana na matatizo ya mimba na uzazi.

4.6.2 Masuala

i. Mahudhurio katika huduma za ujauzito ni ya juu, ambapo asilimia 98 ya wanawake wajawazito hufika katika vyombo vya afya walau mara moja wakati wa ujauzito. Hata hivyo, wengi wao huchelewa kuanza kuhudhuria kliniki; kwa wastani hufika kliniki kwa mara ya kwanza wakati mimba ikiwa ya miezi karibu 5 – 6.

ii. Ubora wa huduma za afya ya uzazi zinazotolewa si wa kuridhisha kwani vituo vingi vinakosa vyombo muhimu, vifaa na huduma za maabara, kama vile, uchunguzi wa kaswende, utoaji ushauri na upimaji wa VVU na ukadiriaji wa uekundu wa damu.

iii. Miundombinu ya vyombo vingi vya afya ni ya hali duni na kuna nafasi isiyotosheleza. Hivyo vinahitaji ukarabati au kujengwa upya kuhakikisha usalama na faragha kwa wateja, na kuwezesha utoaji wa huduma bora.

iv. Kiasi cha wanaojifungua majumbani ni cha juu (asilimia 53 kwa mujibu wa *Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania, 2004-05*); na kiwango cha vifo vya uzazi vya akinamama nacho ni cha juu (578 kwa kila uzazi hai 100,000, *Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania, 2004-05*). Hii huchangiwa na vipengele vingi, ikiwa ni pamoja na ufikikaji duni, mfumo duni wa rufaa na upungufu wa wafanyakazi wenye ujuzi katika vituo vingi vya afya, hususani vijijini.

v. Kuna idadi isiyotosheleza ya vyombo vya afya vinavyotoa huduma za dharura za uzazi, na huduma za baada ya utoaji mimba. Zaidi ya hayo, kuna ugavi usiotosheleza na usio wa hakika wa dawa na vifaa muhimu kwa ajili ya huduma za dharura za uzazi na huduma za baada ya utoaji mimba.

vi. Matumizi ya mbinu za kisasa za uzazi wa mpango bado ni duni (asilimia 20 tu). Pia kuna programu chache za uzazi wa mpango zilizokitwa katika jamii. Kwa mujibu wa *Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania, 2004-05*, mahitaji yasiyokidhiwa ya uzazi wa mpango ni kiasi cha juu cha asilimia 22.

vii Huduma za baada ya kujifungua zinatolewa katika vyombo vichache kutokana na kutokuwepo mwamko wa wateja na watoa huduma kuhusu umuhimu wake. Ni asilimia 5 tu ya wanaojifungua huhudhuria huduma za baada ya kujifungua.

viii. Kuenea kwa ukeketaji ni kwa kiwango cha juu (asilimia 15, *Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania, 2004-05).* Kiasi kinatofautiana kimkoa kutoka chini ya asilimia 1 huko Kigoma hadi asilimia 68 huko Dodoma, na karibu asilimia 81 huko Manyara. Asilimia ya wanawake wanaokeketwa wafikapo umri wa mwaka 1 ni kubwa katika maeneo ya mijini (asilimia 34) kuliko maeneo ya vijijini (asilimia 28); na kiasi cha ukeketaji katika umri wa miaka 13 au baadaye ni asilimia 19 na 31 kwa mijini na vijijini, kwa mfuatano huo. Karibu asilimia 9 ya ukeketaji hufanyika katika umri wa kati ya miaka 15 – 19, asilimia 14 kati ya miaka 20 – 24, asilimia 15 kati ya miaka 25 – 29, na karibu asilimia 26 kati ya umri wa miaka 30 – 39, asilimia 19 kati ya umri wa miaka 40 – 44 na asilimia 23 katika umri wa miaka 45 – 49.

ix. Viwango vya maradhi na vifo vya watoto wachanga na watoto bado ni vya juu. Sababu kuu za vifo vya watoto wachanga ni pamoja na magonjwa ya kuhara, utapiamlo, malaria, ukosefu wa damu mwilini, maambukizi ya njia ya pumzi na VVU na UKIMWI. Kwa mujibu wa Programu ya Kudhibiti Malaria (2000), karibu watoto 80,000 wa umri wa chini ya miaka mitano wanakufa kwa malaria kila mwaka. Programu ya Malaria (2003) inaonyesha kwamba ni asilimia 26 tu ya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano wanatumia vyandarua vilivyotiwa dawa.

x. Chanjo kwa jumla imeenea kwa kiwango cha juu. Nia ni kufikia asilimia 90 ya chanjo zote kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja na kufikia kila wilaya kwa kuwa na utoaji wa Chanjo ya Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda na Homa ya Manjano kwa asilimia 90 katika wilaya zote; na ikiwezekana, kufikia kila wilaya kwa chanjo zote. Kutolewa kwa Chanjo ya Kifua Kikuu ni asilimia 88, Polio ni asilimia 89 na surua ni asilimia 89 (*Mpango wa Taifa wa Chanjo* – 2001). Juhudi za mara kwa mara za kuongeza ubora wa chanjo zinaendelea.

xi. Kuna programu zisizotosheleza za kushughulikia mahitaji ya afya ya uzazi kwa makundi mahsusi ya watu, hususani vijana na wazee. Matokeo yake wanashindwa kupata taarifa na huduma sahihi.

xii. Kuna ushiriki na msaada mdogo kwa wanaume katika masuala ya afya ya uzazi.

4.6.3 Madhumuni ya Sera

i. Kukuza mwamko wa umma kuhusu afya ya ngono na uzazi; na haki kwa vijana, wanaume na wanawake

ii. Kukuza na kupanua ubora wa huduma za afya ya uzazi; na ushauri kwa vijana, wanaume na wanawake

iii. Kukuza matunzo ya afya na huduma kwa watoto wachanga na watoto ili kupunguza magonjwa na vifo vya watoto wachanga na watoto

4.6.4 Mwelekeo wa Sera

i. Kukuza na kupanua upeo wa utetezi wa afya ya uzazi na progamu za Taarifa, Elimu na Mawasiliano

ii. Kukuza ushiriki na kujihusisha kwa jumuiya katika kutoa huduma za afya ya uzazi

iii. Kuimarisha mfumo bora wa utoaji wa huduma za afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na mfumo wa kuhakikisha usalama wa vifaa vya afya ya uzazi

iv. Kuanzisha huduma mahsusi za afya ya uzazi kwa ajili ya vijana na wazee

v. Kutoa huduma za afya ya uzazi pana kushughulikia matatizo ambayo hayajashughulikiwa, ikiwa ni pamoja na matatizo ya uzazi miongoni mwa wanaume na wanawake, saratani za mfumo wa uzazi, huduma za baada ya kuzaa, matatizo ya baada ya kutoa mimba na fistula

vi. Kuboresha ueneaji wa chanjo na kuimarisha usimamizi wa magonjwa ya utotoni

vii. Kukuza hatua za kuondoa mazoea ya kijadi yenye madhara, hususani ukeketaji

viii. Kuwahimiza wanaume kushiriki katika Programu za Afya ya Uzazi

ix. Ubia wa sekta za umma na binafsi kwa ueneaji madhubuti na thabiti wa vyombo na huduma za afya zilizolengwa hasa katika ufikikaji bora

4.7 Magonjwa yanayoenezwa kwa Njia ya Ngono, VVU na UKIMWI

4.7.1 Masuala

i. Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye viwango vya juu vya kuenea kwa VVU na UKIMWI duniani. Inakadiriwa pia kwamba karibu watu milioni 1.81 walikuwa wanaishi na VVU na UKIMWI kufikia 2003 (Ripoti ya 18 ya Ufuatiliaji ya Programu ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI). Jumla (limbikizi) ya idadi ya matukio ya VVU na UKIMWI yaliyoripotiwa tangu matukio 3 ya mwaka 1983 imefikia watu 176,102. Katika jumla hii limbikizi, matukio 18,929 yaliripotiwa katika mwaka wa 2003 peke yake. Idadi ya matukio ya UKIMWI yaliyoripotiwa mwaka 2003 ilikuwa ya juu kuliko ile iliyoripotiwa katika miaka mingine yoyote iliyopita.

ii. Hali hii imetishia kufupisha miaka anayotarajiwa mtu kuishi. Mlipuko huu umekuwa na athari nyingine kubwa kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi; kwani unaendelea kuathiri watu wenye umri wa kuzalisha na kuzaa katika jamii, hususani wa umri wa miaka 20 – 49. Ruwaza ya maradhi huonyesha maambukizi ya mapema kwa wanawake wa umri mdogo na kuongezeka kwa wanawake wa umri wa miaka 25 – 34, wakati kwa wanaume matukio mengi hutokea baadaye kidogo maishani na kuongezeka katika miaka 30 – 39.

iii. Tokeo jingine ni kuongezeka kwa idadi ya watoto yatima ambao kwa wakati huu wanakadiriwa kuwa zaidi ya 800,000.

iv. Kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha maambukizi ya VVU, kuna uwezekano mkubwa wa kuathiriwa kwa muda wa watu kuishi na ubora wa maisha ya vijana nchini Tanzania, hususani wale wa umri wa chini ya miaka 15, ambao ni karibu asilimia 44 ya watu wote. Kundi moja maalumu la watu ni vijana wadogo (umri wa miaka 10 – 19) ambao ni karibu asilimia 22 ya watu wote. Kundi hili lina uwezekano wa kuambukizwa kirahisi VVU kutokana na sababu mbalimbali, ambazo ni pamoja na kushindwa kupata taarifa na huduma za afya ya uzazi; na vilevile masuala ya kijamii, kiuchumi na kijinsia.

v. Umaskini ni kipengele kingine muhimu katika uwezekano wa kuambukizwa kwa urahisi VVU vijana wadogo, hususani msichana mdogo. Viwango vya juu vya maambukizi ya VVU kwa kundi hili vitakuwa na athari kwa tija ya nchi kukabiliana na umaskini na malengo mengine ya kitaifa na ya kiulimwengu kwa muda mrefu ujao.

vi. Usimamizi wa magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya ngono ni hafifu, kwani inatolewa na karibu asilimia 50 tu ya vyombo vya afya. Aidha ni asilimia 22 tu ya vyombo vya afya vinashughulikia uchunguzi wa kaswende wakati wa ujauzito.

4.7.2 Madhumuni ya Sera

i. Kukuza maendeleo na utekelezaji wa hatua za sekta mbalimbali za kukabiliana na VVU na UKIMWI

ii. Kukuza tiba na huduma jumuishi ya Magonjwa yanayoenezwa kwa Njia ya Ngono, VVU na UKIMWI

iii. Kukuza na kusaidia juhudi miongoni mwa jumuiya kuwahudumia watu waishio na VVU na UKIMWI na yatima

4.7.3 Mwelekeo wa Sera

i. Kukuza utekelezaji wa mipango ya kisekta ya VVU na UKIMWI

ii. Kusaidia ushiriki wa sekta binafsi, AZISE na mashirika ya kidini katika utekelezaji wa hatua za kukabili VVU na UKIMWI

iii. Kuongeza ufikiwaji wa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI kupata tiba bora iliyopo na huduma, ikiwa ni pamoja na dawa za kurefusha maisha

iv. Kuimarisha mfumo wa huduma za afya, kutoa na kufuatilia huduma kwa Magonjwa yanayoenezwa kwa Njia ya Ngono, VVU na UKIMWI, ikiwa ni pamoja na dawa za kurefusha maisha

v. Kukuza hatua zinazohakikisha matunzo na huduma nzuri kwa yatima

4.8 Uhifadhi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu

4.8.1 Maliasili

Tanzania imejaliwa kuwa na maliasili nyingi za aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ardhi yenye rutuba, wanyamapori, rasilimali za majini, madini, ardhioevu na mawanda. Karibu asilimia 50 ya ardhi yote ya Tanzania imefunikwa na misitu na mapori, asilimia 40 ya mbuga na vichaka na ni asilimia 6 – 8 tu inayolimwa. Rasilimali za maji ni pamoja na maziwa Viktoria, Tanganyika na Nyasa, na maziwa mengine madogo madogo ndani ya nchi; ukanda wa pwani, mito, vinamasi, mabonde tambarare yanayounda rasilimali ya ardhioevu. Rasilimali ya bahari ni pamoja na samaki, miamba tumbawe, fukwe za mchanga, mikoko, nyasi za baharini, rasilimali ya chumvi na bioanuwai nyingine. Wanyamapori ni sehemu muhimu ya majaliwa ya rasilimali ya Tanzania; karibu asilimia 25 ya ardhi yote ni maeneo yanayolindwa, ikiwa ni pamoja na hifadhi za misitu. Maeneo haya yanayolindwa huunda maeneo makuu ya utalii. Rasilimali kuu za nishati ni viumbe hai katika eneo (biomasi), nguvu za maji na makaa ya mawe. Kuna uwezekano pia wa kuwepo gesi ya asili, nishati ya jua na nishati ya upepo.

4.8.2 Masuala

i. Msingi wa maliasili unaendelea kupungua. Sababu za kupungua huku ni pamoja na ukataji miti, mifugo inayozidi malisho, uchafuzi, kupotea kwa bioanuwai, mazoea mabaya ya kilimo na mwamko mdogo kuhusu mazingira. Vipengele vingine vinavyochangia ni pamoja na ukuaji wa idadi ya watu na rasilimali ya fedha isiyotosheleza. Kutojumuishwa vya kutosha kwa masuala ya mazingira katika mchakato wa kibinadamu, kiteknolojia na kimipango pia kunachangia katika kupungua kwa msingi wa maliasili.

ii. Maji, kama rasilimali, ni muhimu katika kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii endelevu na kwa kutunza ubora wa mazingira.

Tanzania inayo rasilimali kubwa ya maji; lakini rasilimali hiyo imesambaa kwa namna isiyolingana katika wakati, nafasi na kiasi; na yenye kutofautiana sana katika ubora na kusababisha vikwazo na mapungufu kwa maendeleo. Maji salama ya kunywa na mazoea mazuri ya usafi ni masharti muhimu kwa afya ya binadamu.

iii. Huduma za ugavi wa maji nchini ni za chini. Kuenea kwake katika mwaka 2003 kulikuwa asilimia 53 kwa watu wa vijijini na asilimia 73 kwa watu wa mijini. Ingawa vipimo vya kitakwimu vimekitwa katika uwezo wa uwekwaji, inakadiriwa kwamba zaidi ya asilimia 30 ya miradi ya maji vijijini haifanyi kazi vizuri kutokana na mipango duni ya uendeshaji na matunzo. Hali hizi zinasababishwa na kuvuja kwingi kutokana na ukuukuu, ukosefu wa matunzo mazuri na ya mara kwa mara ya mifumo ya ugavi wa maji; na vilevile gharama kubwa za uendeshaji kwa kutumia umeme na mafuta kusukuma maji. Zaidi ya hayo, baadhi ya huduma za ugavi maji mijini hazitiwi dawa vizuri kwa sababu ya mitambo mibovu ya utiaji dawa.

iv. Matatizo makubwa yanayoathiri huduma za maji na usafi nchini Tanzania ni pamoja na fedha zisizotosha za kujenga mifumo mipya na matunzo ya mifumo iliyopo ya maji safi na majitaka, kuharibiwa kwa vyanzo vya maji na kutokuzwa kwa kiasi cha kuridhisha kwa mbinu za kuvuna maji. Makazi yasiyopangwa na kusongamana mijini vinachangia katika kutopatikana kwa kiasi cha kuridhisha cha maji safi na salama na huduma za utupaji wa majitaka na takangumu.

4.8.3 Madhumuni ya Sera

i. Kuongeza upangaji mipango jumuishi, matumizi endelevu na usimamizi imara wa maliasili

ii. Kuongeza mgao wa kimgaosawa wa maji safi na salama katika maeneo ya vijijini na mijini

iii. Kuongeza fahiwa ya umiliki na utamaduni wa kutunza miundombinu

4.8.4 Mwelekeo wa Sera

i. Kukuza mkabala jumuishi wa upangaji mipango na usimamizi wa maliasili

ii. Kujumuisha tafakuri za kimazingira katika programu na mipango ya maendeleo

iii. Kuzuia na kudhibiti uharibifu wa mazingira

iv. Kujenga mifumo mipya na ya kuaminika ya maji na usafi

v. Kukarabati na kutunza miundombinu iliyopo

vi. Kutafuta na kutumia vyanzo vipya na kukuza matumizi endelevu ya rasilimali iliyopo

vii. Kukuza matumizi ya mamlaka na udhibiti pamoja na vyombo vya uchumi kwa usimamizi wa mazingira na maliasili

viii. Kukuza matumizi ya vyanzo vingine vya nishati kupunguza shinikizo kwenye vyanzo vya nishati ya viumbe hai (biomasi)

4.9 Kilimo, Chakula na Lishe

4.9.1 Kilimo kinabakia kuwa sekta moja muhimu katika uchumi kutokana na mchango wake kwa Pato la Taifa la Ndani, utoaji wa ajira na kupunguza umaskini. Hata hivyo, katika miaka yote ya utendaji wake, sekta hii imekuwa ikibadilikabadilika lakini mara zote imebakia chini ya viwango ambavyo vingependelewa.

4.9.2 Masuala

i. Uzalishaji wa kilimo umekuwa ukibadilikabadilika kutokana na vipengele kadhaa, ikiwa ni pamoja na sehemu yake kubwa kuwa kilimo cha wakulima wadogowadogo kinachotegemea mvua ambayo yenyewe si ya kuaminika.

ii. Kuna matumizi madogo tu ya kilimo cha umwagiliaji. Tanzania ina vyanzo vingi vya maji ambavyo havitumiwi kwa umwagiliaji. Wakulima wadogowadogo hawajawezeshwa kwa kupewa stadi na vyombo ambavyo vingewawezesha kuongeza tija na uzalishaji.

iii. Nchi haijaweza kuzalisha chakula cha kutosha kwa matumizi. Hii inadhihirishwa na kutokea kwa njaa nchini muda hadi muda katika miongo kadhaa.

iv. Utapiamlo miongoni mwa watoto chini ya miaka mitano bado uko juu; na hakuna mabadiliko muhimu katika viwango vya utapiamlo vilivyochunguzwa katika muongo uliopita. Kwa mujibu wa *Uchunguzi wa Hali ya Uzazi na Afya ya Mtoto, 1999*, karibu asilimia 44 ya watoto wamedumaa, asilimia 5 wamedhoofu na asilimia 29 wana uzito wa chini. Asilimia 95 ya watoto wananyonyeshwa; wastani wa muda wa kunyonyeshwa ukiwa miezi 21. Hata hivyo, wastani wa muda wa kunyonya tu ni mwezi mmoja tu, ukiakisi kuanzishwa mapema kwa vyakula vingine kwa mtoto kunakochangia kuleta magonjwa ya kuhara na utapiamlo.

v. Kukosekana au viwango vya chini vya mwamko na elimu ya lishe kwa sehemu kubwa ya watu

4.9.3 Madhumuni ya Sera

i. Kuongeza uzalishaji wa chakula na kuhakikisha kuwepo uhakika wa chakula
ii. Kuongeza miradi ya umwagiliaji
iii. Kupunguza kabisa upotevu wa kabla na baada ya mavuno na kuboresha uhifadhi wa chakula
iv. Kuboresha hadhi ya lishe ya wanawake, wanaume na watoto

4.9.4 Mwelekeo wa Sera

i. Kuhakikisha kuwepo uhakika wa chakula katika ngazi za taifa na kaya
ii. Kukuza mazoea ya kisasa ya kilimo; ikiwa ni pamoja na umwagiliaji na kuboresha teknolojia na miundombinu sahihi ya kilimo
iii. Kutoa mikopo kwa wakulima wadogowadogo
iv. Kuhakikisha upatikanaji na umiliki wa ardhi kwa wakulima wadogowadogo
v. Kuongeza elimu ya chakula na lishe kwa jamii
vi. Kuondoa vipingamizi vya kiutamaduni ili kuboresha hadhi ya lishe
vii. Kudhibiti upungufu wa viinilishe na viinilishe vya protini
viii. Kukuza usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo na kupunguza upotevu unaotokea baada ya mavuno
ix. Kusaidia utafiti wa kubuni teknolojia nafuu zinazopunguza mzigo wa kazi kwa wanawake

4.10 Umaskini nchini Tanzania

4.10.1 Masuala

i. Kwa mujibu wa uchanganuzi wa *Utafiti wa Bajeti ya Kaya, 2000/01* na *Utafiti wa Nguvukazi Jumuishi, 2000/01*, Tanzania bado ina sehemu kubwa ya watu wanaoishi chini ya kiwango cha umaskini. Sehemu ya watu wasioweza kumudu mahitaji ya msingi ya chakula ni asilimia 19 ya watu wote. Hata hivyo, sehemu ya watu wenye mapato yasiyotosheleza mahitaji ya msingi (yaani chakula, nyumba, mavazi, elimu ya msingi kwa watoto na huduma muhimu za afya) ni asilimia 36. Hali hii inapolinganishwa na ile katika *Utafiti wa Bajeti ya Kaya, 2000/01*, kumekuwa na maendeleo kidogo yanayojidhihirisha katika maeneo ya mijini, hususani jiji la Dar es Salaam; lakini hali katika maeneo ya vijijini imebakia karibu vilevile.
ii. Uchanganuzi zaidi unadhihirisha kwamba asilimia 17 ya maskini wote wanaishi katika maeneo ya vijijini, ukilinganisha na asilimia 13 katika maeneo ya mijini. Kuna uhusiano wa karibu kati ya hadhi ya umaskini na kiwango cha elimu cha kiongozi wa kaya. Asilimia 51 ya maskini walikutwa katika kaya zenye viongozi ambao hawakupata elimu ya msingi kwenda juu.

Zaidi ya hayo, uchanganuzi unaonyesha kwamba kaya zinazotegemea kilimo, hususani kilimo cha kujikimu, zina viwango vya juu vya umaskini. Kiwango hiki huongezeka miongoni mwa kaya zenye wanakaya wengi na ambao viongozi wao hawana shughuli za uchumi wala elimu ya msingi.

iii. Kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii, uchanganuzi unabaini kwamba watu maskini wanadhurika zaidi. Sehemu ya wanafunzi wa shule za msingi kutoka kaya maskini ni ndogo sana na imekuwa ikishuka katika miaka ya 1990. Upatikanaji wa huduma za afya kwa watu maskini pia unashuka kutokana na msingi wao mdogo wa rasilimali. Aidha, watu wengi hutumia maji yasiyo salama na asilimia 54 ya kaya maskini hutegemea vyanzo visivyolindwa vya maji ukilinganisha na asilimia 40 tu ya kaya zinazojiweza.

4.10.2 Madhumuni ya Sera

i. Kuondoa umaskini wa kutupwa
ii. Kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii

4.10.3 Mwelekeo wa Sera

i. Kudumisha uimara wa uchumi kwa kuhakikisha umadhubuti wa soko, msaada wa bajeti kwa utoaji wa huduma za kijamii na upanuzi wa hatua za kuwapendelea maskini katika sekta tofauti
ii. Kukuza maendeleo ya sekta ya maeneo ya vijijini na ukuaji wa bidhaa za kuuzwa nje
iii. Kukuza maendeleo ya sekta binafsi
iv. Kuboresha thamani ya uwezo wa binadamu kwa kutoa elimu inayofaa
v. Kuwawezesha watu kuongeza msingi wao wa kiuchumi

4.11 Elimu

4.11.1 Masuala

i. Uandikishaji wa wanafunzi wa shule za msingi umekuwa ukibadilikabadilika. Uandikishaji wa jumla umeshuka kutoka asilimia 90 mnamo 1982 hadi asilimia 74 mnamo miaka ya 1990; na ulipanda tena kufikia asilimia 109.9 mnamo 2005 kufuatia kuanzishwa kwa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Kiwango cha uhitimu wa shule za msingi pia ni cha chini ikilinganishwa na shabaha ya Taifa. Mnamo 2004 kilikuwa asilimia 72.
ii. Uwezo wa Tanzania wa elimu bado unatoa fursa chache kwa vijana baada ya

kumaliza elimu ya msingi. Mpito hadi shule ya sekondari (2004) ni asilimia 36.1 tu ya wanafunzi wote waliomaliza darasa la VII. Asilimia 63.9 inayobaki ya waliomaliza shule za msingi mwaka 2004 hawakuweza kwenda shule za sekondari. Asilimia 63.9 ya wanafunzi waliomaliza shule za msingi ambao hawaendi shule za sekondari wanalazimishwa kuingia katika maisha ya utu uzima wakiwa wangali wadogo sana. Kuhusiana na uwiano wa kijinsia, idadi ya wasichana na wavulana ni karibu sawa katika ngazi ya msingi; lakini kuna wavulana wengi kuliko wasichana katika ngazi ya sekondari na ya elimu ya juu.

iii. Elimu ya watu wazima iliyofikia kilele chake katika miaka ya mwanzo ya 1970 imeshuka hadi chini kabisa mnamo 2003. Hii, pamoja na mielekeo isiyopendezeka katika ngazi ya shule za msingi, imechangia katika kiwango kinachoongezeka cha kutojua kusoma na kuandika.

4.11.2 Madhumuni ya Sera

i. Kuhamasisha sekta binafsi, AZISE na mashirika ya kidini kuwekeza katika utoaji wa elimu

ii. Kukuza utoaji wa elimu kimgaosawa, na wa kuweza kugharimiwa na bora kwa wavulana na wasichana

4.11.3 Mwelekeo wa Sera

i Kuhimiza ushiriki wa jamii katika utoaji wa elimu bora

ii. Kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi, AZISE na mashirika ya kidini kuwekeza katika utoaji wa elimu

iii. Kukuza mgaosawa wa fursa za elimu ili kurekebisha upogo kijinsia na kimkoa

iv. Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza

v. Kutoa elimu ya msingi kwa watoto wote wa umri wa kwenda shule

vi. Kupunguza kiwango cha kutojua kusoma na kuandika kwa watu wazima

4.12 Ukusanyaji, Uchakataji, Uhifadhi, Usambazaji wa Data, Mafunzo na Utafiti

4.12.1 Masuala

i. Katika miaka mingi ya hivi karibuni, Tanzania imeshuhudia kuzidi kutambuliwa kwa haja ya data za kitakwimu sahihi, pana na za wakati huo zaidi. Msukumo wa kuboresha shughuli za ukusanyaji data za Serikali umetoka kwa Wizara moja moja ambazo zimezidi kubaini kuwa uchunguzi wa kina wenye changanuzi za kiidadi na kithamani, ni muhimu kwa

mchakato wa ufanyaji maamuzi wa kitaifa na upangaji mipango madhubuti; lakini watumiaji wa data hawaweki rasilimali za kutosha kwa zoezi la ukusanyaji data. Sensa za idadi ya watu zimebakia kuwa vyanzo vikuu vya data za idadi ya watu. Hata hivyo, zimesaidiwa na tafiti za kitaifa zikiwemo *Utafiti wa Hali ya Afya na Uzazi Tanzania, 1973*, T*afiti za Hali ya Afya na Uzazi Tanzania* zilizofanywa 1991/92, 1996 na 2004/05 na *Uchunguzi wa Hali ya Uzazi na Afya ya Mtoto*, 1999. Katika tafiti hizi makisio ya demografia yanayohusiana mahsusi na uzazi na vifo, na vilevile uzazi wa mpango na data zinazohusiana na afya zilipatikana.

ii. Kwa muda mrefu sasa mipango ya maendeleo nchini Tanzania imeathiriwa kwa namna hasi na tatizo linaloendelea la ukosefu wa data za kutosha, za kuaminika na za wakati unaohusika. Mpaka sasa nchi haina uwezo wa kutosha wa kukusanya, kuchakata, kuchanganua, kuhifadhi na kusambaza data. Mifumo iliyopo ya uzalishaji na usimamizi wa data nchini ni hafifu. Rasilimali inayogawiwa kwa ajili ya ukusanyaji na usimamizi wa data mara nyingi zimekuwa hazitoshi na hii imeelekea kuendeleza tatizo la data. Wakati utafiti ni kazi muhimu katika uzalishaji wa data zinazohitajika kwa upangaji mipango, hii imekuwa ni mojawapo ya maeneo yaliyonyimwa rasilimali. Zaidi ya hayo, utafiti mdogo unaofanywa hauratibiwi vizuri wala matokeo yake hayawekewi kumbukumbu na kusambazwa kwa namna ya kuridhisha.

iii. Mafunzo katika mitaala ya demografia na idadi ya watu yalianzishwa katika asasi za elimu ya juu mwishoni mwa miaka ya 1980. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma vimekuwa vikitoa kozi za demografia na idadi ya watu katika ngazi mbalimbali; na hivi karibuni vimejumuisha mada ya jinsia. Hata hivyo, fedha zilizotolewa kwa programu hizi za mafunzo hazitoshelezi.

4.12.2 Madhumuni ya Sera

i. Kuboresha ukusanyaji, uchakataji, uchanganuzi, uhifadhi na usambazaji wa data za idadi ya watu

ii. Kuboresha utafiti na mafunzo katika masuala ya idadi ya watu

4.12.3 Mwelekeo wa Sera

i. Kuimarisha juhudi katika ukusanyaji, uchakataji, uchanganuzi, uwekaji kumbukumbu na usambazaji kwa wakati unaohusika wa taarifa za idadi ya watu

ii. Kukuza matumizi ya taarifa ya idadi ya watu katika upangaji mipango

iii. Kutoa programu ya mafunzo kwa wafanyakazi kwenye nyanja za ukusanyaji, uchanganuzi wa data na utafiti katika idadi ya watu na maendeleo

iv. Kukuza mafunzo ya stadi mahali pa kazi katika masuala ya idadi ya watu

4.13 Utetezi na Taarifa, Elimu na Mawasiliano

4.13.1 Masuala

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya 1992 haukuwa na mafanikio muhimu, hususani katika maeneo ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, na ujumuishaji wa vigeu vya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo. Hii ni kwa kuwa utetezi haukusisitizwa.Utetezi na Taarifa, Elimu na Mawasiliano yanahitaji kutumiwa na waigizaji ili kuathiri mabadiliko ya mitazamo na kukuza mabadiliko ya tabia katika masuala ya idadi ya watu na si suala la mwamko peke yake.

4.13.2 Madhumuni ya Sera

Kuunda mazingira yenye kuwezesha yatakayorahisisha kukubaliwa kwa masuala ya idadi ya watu

4.13.3 Mwelekeo wa Sera

i. Kuratibu juhudi za utetezi wa idadi ya watu zinazofanywa na Serikali na Washirika wa maendeleo ili kuhakikisha uthabiti katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu

ii. Kukuza mjadala kuhusu masuala ya idadi ya watu miongoni mwa waunda sera na wafanya maamuzi

iii. Kuimarisha ushiriki wa AZISE katika kutetea masuala ya idadi ya watu

iv. Kuanzisha kiunzi cha kiasasi kuratibu Taarifa, Elimu na Mawasiliano ya idadi ya watu na shughuli za utetezi kupitia watu binafsi, makundi na vyombo vya habari

v. Kuongeza ubora wa utetezi na hatua za Taarifa, Elimu na Mawasiliano kwa kujenga uwezo na kubuni vifaa vya Taarifa, Elimu na Mawasiliano vyenye kukubalika kiutamaduni

SURA YA TANO

5.0 MIPANGO YA KIASASI NA DHIMA ZA SEKTA

5.1 Mipango ya Kiasasi

Kwa kiasi kikubwa, Serikali, vyama vya kiraia na sekta binafsi ndivyo vitatekeleza Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Juhudi zitafanywa kuimarisha baadhi ya mawakala watekelezaji kwa njia ya kuwajengea uwezo. Mahsusi kabisa, mawakala watekelezaji wa serikali watakuwa ni pamoja na wafuatao: Baraza la Tanzania la Idadi ya Watu na Maendeleo, Kamati ya Kiufundi ya Taifa ya Idadi ya Watu na Ofisi za masuala ya Idadi ya Watu katika Wizara zote zenye kuhusika na katika ngazi za mikoa na wilaya. Mawakala watekelezaji na dhima zao ni kama inavyoonyeshwa hapa chini.

5.1.1 Baraza la Tanzania la Idadi ya Watu na Maendeleo

Baraza la Tanzania la Idadi ya Watu na Maendeleo litakuwa mratibu mkuu na chombo cha ushauri wa utekelezaji wa sera. Wajumbe wake watakuwa ni Makatibu Wakuu wa Wizara zinazohusika; na Mwenyekiti wao atakuwa ni Waziri mwenye dhamana ya Mipango Jumla. Wajumbe wengine watakuwa ni watendaji wa asasi zinazohusika, yaani, Chama cha Wabunge wa Tanzania cha Masuala ya Idadi ya Watu na Maendeleo, AZISE, Kundi la Wabunge la Masuala ya VVU na UKIMWI na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI. Baraza la Tanzania la Idadi ya Watu na Maendeleo litakutana walau mara moja kwa mwaka. Baraza hilo litakuwa na shughuli zifuatazo.

i. Kushauri kuhusu mikakati ya utekelezaji wa Sera
ii. Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu
iii. Kuidhinisha programu za muda mrefu za idadi ya watu na ripoti za utekelezaji wa sera za kila baada ya miaka miwili
iv. Kushauri kuhusu udurusu wa sera na kupendekeza uthibitisho wa sera ya idadi ya watu iliyodurusiwa

5.1.2 Kamati ya Kiufundi ya Taifa ya Idadi ya Watu

Kamati ya Kiufundi ya Taifa ya Idadi ya Watu ambayo imekuwepo tangu mwaka 1983, ni kamati ya ufundi ya sekta na taaluma mbalimbali. Kamati, miongoni mwa mambo mengine, itatoa msaada wa kiufundi kwa wizara inayohusika na mipango katika ubunifu na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Italishauri Baraza

kuhusu mambo yote yanayohusu idadi ya watu na maendeleo. Kamati itakuwa na wafanyakazi waandamizi wa kiufundi kutoka asasi wadau, na itafanya mkutano walau mara moja kila robo mwaka. Pia kamati ina mamlaka ya kuunda kamati ndogondogo mahali na wakati inapotokea haja.

Kamati itatoa ushauri katika maeneo yafuatayo.

i. Ukusanyaji na uchanganuzi wa kazi zote za utafiti kuhusu idadi ya watu na maendeleo zilizofanywa Tanzania, manufaa yake na usambazaji wa taarifa zilizopatikana kwenda kwenye ofisi za mipango katika sekta na wilaya mbalimbali
ii. Kuandaa na kufanya utafiti kwa malengo ya mipango ya maendeleo
iii. Utunzaji na uendeshaji madhubuti wa kanzi ya data za idadi ya watu
iv. Mifano ya mipango ya idadi ya watu na maendeleo ya baina ya sekta
v. Programu za mafunzo, ikiwa ni pamoja na warsha kuhusu ujumuishaji wa masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo
vi. Uratibu wa utekelezaji wa programu za idadi ya watu na maendeleo

5.2 Dhima na Majukumu ya Wadau

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi Watu unahitaji mkabala wa sekta mbalimbali. Kwa msingi huu, wizara za Serikali na asasi nyingine zitahusika. Dhima na kazi za wizara hizo zinaorodheshwa katika sehemu 5.2.1 – 5.2.21.

5.2.1 Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji/Wizara ya Fedha na Masuala ya Kiuchumi (SMZ)

i. Kuratibu, kufuatilia na kutathmini shughuli na programu zote za idadi ya watu
ii. Kuandaa na kutoa miongozo ya kujumuisha matatizo ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo katika ngazi ya taifa, mikoa na serikali za mitaa
iii. Kushirikiana na wadau wengine katika mambo yanayohusu idadi ya watu na maendeleo endelevu
iv. Kukusanya, kusambaza na kukuza matumizi ya data za idadi ya watu
v. Kuratibu AZISE zinazoshughulika na masuala ya idadi ya watu
vi. Kushirikiana na wadau wengine katika kuhamasisha rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu
vii. Kuandaa programu zinazokuza haki za kijamii na kupunguza umaskini kwa ukuaji endelevu wa uchumi
viii Kufanya utafiti wa mikakati ya kuondoa umaskini

5.2.2 Ofisi ya Makamu wa Rais

i. Kukuza utafiti kuhusu uhifadhi wa mazingira
ii. Kuibua mwamko na kuhisisha umma kuhusu matatizo ya mazingira kupitia vyombo vya habari binafsi na vya umma

5.2.3 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

i. Kuhakikisha kwamba Sera inasambazwa na kueleweka katika ngazi ya wilaya
ii. Kuhakikisha kwamba masuala ya idadi ya watu yanajumuishwa kikamilifu katika mipango na programu za maendeleo za wilaya
iii. Kuhakikisha kwamba masuala ya mazingira yanajumuishwa katika elimu rasmi na isiyo rasmi katika ngazi zote

5.2.4 Ofisi ya Waziri Mkuu

i. Kuratibu juhudi za sekta mbalimbali kwa uzuiaji na udhibiti wa VVU na UKIMWI
ii. Kuratibu uhamasishaji wa rasilimali kwa hatua za kukabiliana na VVU na UKIMWI
iii. Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Sekta Mbalimbali wa VVU na UKIMWI
iv. Kuratibu masuala, shughuli na mambo yote yanayohusu majanga na usimamizi wa majanga

5.2.5 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

i. Kuratibu utekelezaji wa programu za afya ya uzazi
ii. Kushirikiana na asasi nyingine za umma na binafsi katika kutoa huduma za afya ya uzazi
iii. Kuweka viwango na miongozo ya utoaji huduma na kwa watoa huduma za afya
iv. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya katika ngazi zote, na vilevile kuhakikisha kwamba elimu ya afya inaingizwa kwenye mitaala ya asasi zinazotoa mafunzo ya afya
v. Kufanya utafiti kwa kushirikiana na asasi au mawakala wengine kuhusu masuala ya afya ya uzazi
vi. Kuratibu na kutekeleza vipengele vya kiafya vya programu za Magonjwa yanayoenezwa kwa Njia ya Ngono, VVU na UKIMWI
vii. Kwa njia ya Mfumo wa Taarifa za Afya, kukusanya na kutumia data na taarifa za kijinsia zilizotenganishwa
viii. Kutoa usimamizi wa ufuatiliaji na wa usaidizi wa programu za afya ya uzazi

5.2.6 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

i. Kujumuisha Elimu ya Maisha ya Familia katika shule zote za binafsi na za umma za msingi na sekondari, na vyuo vya ualimu
ii. Kusaidia ushiriki wa jumuiya, asasi na sekta binafsi katika utoaji wa elimu kimgaosawa na bora
iii. Kuimarisha utetezi na uhamasishaji wa kijamii wa mgaosawa, usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake
iv. Kuhakikisha utoaji wa elimu ya msingi kwa watoto wote
v. Kuimarisha programu za kujua kusoma na kuandika

5.2.7 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

i. Kuhakikisha kwamba vigeu vya idadi ya watu vinajumuishwa katika programu za mafunzo ya wafanyakazi wa ugani ili kuwapa stadi muhimu, kuwawezesha kuhusisha ukuaji wa idadi ya watu na viwango vya uzalishaji na matumizi ya chakula, na shughuli nyingine za maendeleo katika ngazi za mahali husika
ii. Kukuza matumizi ya vifaa bora vya kilimo, mbinu na mazoea ya kilimo cha kisasa na usindikaji bora wa chakula, na vyombo vya uhifadhi
iii. Kuhakikisha uhakika wa chakula kwa taifa

5.2.8 Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

i. Kukuza programu za vijana kwa ajili ya kuwafanya kuwa wazazi wenye kuwajibika
ii. Kukuza kwa ushirikiano na asasi nyingine, fursa za ajira, hususani kwa vijana na watu wenye ulemavu
iii. Kuanzisha sheria pana za ajira zitakazohimiza mahusiano shirikishi ya ajira katika sekta za umma na binafsi
iv. Kuimarisha mabaraza ya vijana na kamati za maendeleo
v. Kukuza ustawi wa wazee na makundi yenye matatizo

5.2.9 Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

i. Kuhimiza vyombo vya mawasiliano ya kijamii na mabaraza ya thieta za kisasa kuhusu dhamira zenye kuhusiana na idadi ya watu na maendeleo

5.2.10 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

i. Kutetea mgaosawa, usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa wanawake na haki za watoto
ii. Kuelimisha wanawake kuhusu umuhimu wa kunyonyesha, uzazi salama na uzazi wa mpango

iii. Kuhakikisha kwamba umuhimu maalumu unawekwa kwa programmu zinazoelekezwa katika kuondoa mazoea ya kijamii na kiutamaduni na ya kiubaguzi dhidi ya wasichana, wazee na watu wenye ulemavu

iv. Kushirikana na wadau wengine katika kuwaelimisha wanawake, wanaume na watoto kuhusu haki zao

v. Kuhakikisha kuwa jinsia inaingizwa katika sera, progamu na mipango

vi. Kubainisha sheria zenye kubagua

vii. Kuwahisisha wanawake, wanaume na watoto kuhusu uondoaji wa mazoea ya kijamii na kiutamaduni yenye madhara

viii. Kuhakikisha kwamba maafisa wa maendeleo ya jamii wanapatiwa utaalamu unaohitajika

5.2.11 Wizara ya Maji

i. Kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wote

5.2.12 Wizara ya Fedha

i. Kuhamasisha rasilimali za ndani na za nje ya nchi ili kusaidia programu na shughuli za idadi ya watu

ii. Kugawa rasilimali za fedha kwa shughuli na progamu za idadi ya watu

5.2.13 Wizara ya Mambo ya Ndani

i. Kuratibu masuala ya uhamaji

ii. Kusimamia na kuratibu masuala ya wakimbizi

5.2.14 Wizara ya Usalama wa Raia

i. Kudumisha uzingatifu wa sheria na utulivu

ii. Kupunguza viwango vya uhalifu

5.2.15 Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba

i. Kushirikiana na Wizara nyingine zote kuhakikisha kuwa sheria ambazo haziendani na Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ama zinapitiwa au kufutwa, na vilevile kuwezesha utungaji wa sheria mpya zinazohusu masuala ya idadi ya watu, afya ya uzazi, mazingira na masuala mengine ya idadi ya watu

ii. Kuhakikisha utekelezaji wa sheria za nchi

5.2.16 Wizara ya Nishati na Madini

i. Kukuza matumizi na utafiti juu ya rasilimali za nishati zinazojizalisha
ii. Kuibua mwamko wa jamii kuhusu hatari za uharibifu wa mazingira katika vipengele vinavyohusiana na utoaji wa nishati kama vile umeme na kuni

5.2.17 Asasi za Elimu ya Juu

i. Kutoa mafunzo kuhusu idadi ya watu na maendeleo
ii. Kufanya utafiti kuhusu masuala yote yenye kuhusiana na idadi ya watu na maendeleo
iii. Kutoa ushauri wa kitaalamu na huduma za ushauri kuhusu masuala ya idadi ya watu na maendeleo
iv. Kujumuisha masuala ya jinsia katika mitaala iliyopo

5.2.18 Vyombo vya Habari

i. Kukuza mwamko kuhusu masuala ya idadi ya watu, sera na programu kuhusiana na maendeleo
ii. Kukuza matumizi ya huduma za afya ya uzazi
iii. Kuarifu na kuelimisha umma kuhusu matatizo ya idadi ya watu, kama vile, dhuluma za kijinsi, VVU na UKIMWI, vurugu za majumbani, kuacha na kutelekeza watoto na vijana wadogo

5.2.19 AZISE na Sekta Binafsi

i. Kutoa huduma za afya ya uzazi
ii. Kutoa huduma za ushauri, hususani kwa vijana, wazee, watu wenye ulemavu na watu wenye mahitaji maalumu
iii. Kusaidia juhudi za Serikali katika mipango, fedha, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya programu za idadi ya watu
iv. Kutoa msaada wa kiufundi na kifedha katika kubuni programu na miradi iliyokitwa katika maendeleo ya idadi ya watu

5.2.20 Vyama vya Siasa

i. Kusaidia ujumuishaji wa masuala ya idadi ya watu katika ajenda ya kijamii na maendeleo
ii. Kuhisisha umma kuhusu masuala ya idadi ya watu na kuhamasisha msaada kwa ajili ya programu za idadi ya watu

5.2.21 Asasi za Kidini

i. Kutoa mwongozo wa kiroho na kuweka viwango vya amali za jamii za uadilifu
ii. Kutoa, kubuni na kutekeleza miradi inayosaidia juhudi zinazofanywa na wengine
iii. Kusaidia juhudi za serikali katika programu zenye kuhusiana na idadi ya watu kwenye maeneo yao

SURA YA SITA

6.0 UPANGAJI MIPANGO, UFUATILIAJI NA TATHMINI

6.1 Utangulizi

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu unahitaji ushiriki madhubuti wa sekta mbalimbali ili kuhakikisha kwamba idadi ya watu na maendeleo zinasaidiana na kuunganika kikamilifu. Dhima shirikishi ya Wizara za kisekta, Idara, Mawakala, sekta binafsi na vyama vya kiraia ni muhimu katika kufanikisha madhumuni yaliyotajwa ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Athari inayotarajiwa ya sera nzuri ya idadi ya watu inaakisiwa kwenye ukuaji wa kasi na uchumi endelevu na maendeleo ya taifa, ambayo kwa upande wake, huwezesha utoaji wa huduma za msingi za kijamii kwa watu. Kwa sababu hii sera ya idadi ya watu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi hayatenganishiki na, kwa hakika, yanaathiriana.

6.2 Urazini wa Upangaji Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni sehemu muhimu katika mchakato wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Hizi zinafuatilia maendeleo ya utekelezaji ambayo yanawawezesha wadau kufanya maamuzi mazuri ili kufanikisha madhumuni yaliyotajwa na kuonyesha matokeo ya uwajibikaji. Kwa hiyo, kazi yao inapaswa kuwa sehemu kamili ya mchakato wote wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu.

6.3 Kiunzi cha Upangaji Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini

Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu inalenga kufanikisha madhumuni, malengo na shabaha zilizowekwa. Sera pia imebainisha maeneo ya kipaumbele ya kushughulikiwa ili kufanikisha malengo, madhumuni na shabaha za sera zilizotajwa. Baadhi ya hizi zinaweza kufanikishwa katika muda mrefu, baadhi katika muda wa kati na nyingine katika muda mfupi. Kama hali ilivyo wakati wote, ufanikishaji wa malengo, madhumuni na shabaha za sera za muda mrefu na muda wa kati unategemea sana mambo yanavyofanyika katika muda mfupi. Vilevile, kama sera ni ya sekta mbalimbali katika upeo na maudhui, utekelezaji wake utafanyika kwa kutekeleza sera na programu nyingine kadhaa za sekta, zikiwa ni pamoja na zile za afya, chakula, ajira, jinsia, upunguzaji umaskini, VVU na UKIMWI, n.k. kwa kuyataja machache tu. Kwa maneno mengine, utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu utahusu wahusika kadhaa katika sekta mbalimbali. Ili kuhakikisha kuwa mawakala wahusika wote wanatenda inavyopasa, uratibu wa juhudi za malengo ya asasi husika, ufuatiliaji wa utekelezaji wa hatua mbalimbali na tathmini ya utendaji ni muhimu mno.

6.4 *Maeneo ya kazi ya kipaumbele ya ufuatiliaji na tathmini*

i. Ujumuishaji wa vigeu vya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo
ii. Ajira
iii. Matatizo ya makundi maalumu katika jamii
iv. Mgaosawa, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake
v. Afya ya ngono na uzazi
vi. Magonjwa yanayoenezwa kwa Njia ya Ngono, VVU na UKIMWI
vii. Uhifadhi wa mazingira
viii. Kilimo, chakula na lishe
ix. Umaskini
x. Elimu
xi. Usimamizi wa data
xii. Utetezi na Taarifa, Elimu na Mawasiliano

6.5 *Viashirio vya Ufuatiliaji na Tathmini*

Kwa msingi wa maeneo ya kazi ya kipaumbele yaliyotajwa hapo juu, utekelezaji wa Mpango wa Kazi utabuniwa. Ubunifu wa mpango wa kazi pia utajumuisha ubunifu wa viashirio vitakavyotumika kufuatilia maendeleo ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Viashirio vinavyohitajika pia vitabuniwa kwa msingi wa maeneo ya kipaumbele ya sera ya ufuatiliaji na tathimini. Kwa kuwa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu unahusu na utahusu wahusika wengi, kila mmoja wao atabuni na kutumia viashirio vya utumiaji vinavyohitajika kwa ufuatiliaji wa maendeleo kwenye maeneo ya mamlaka ya mhusika. Kwa mfano, kuhusiana na uondoaji umaskini, asasi inayoratibu yenye mamlaka (kwa wakati huu Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji) inatarajiwa kubuni viashirio vya ufuatiliaji kwa eneo hilo. Kwa bahati nzuri, viashirio vya ufuatiliaji vinavyohitajika kwa maeneo mengi ya kazi ya kipaumbele tayari vipo. Ila tu mapitio na uboreshaji yanaweza kuhitajika kadiri hali na vipaumbele vitakavyoamua.

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ina wahusika wengi wenye dhima na uwezo vinavyotofautiana. Hawa washirika watekelezaji wanahitaji mpango wa kiasasi wa uratibu na wa kutumia taarifa pamoja. Lengo la mwisho la matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ni kuhakikisha ufanisi, uthabiti na uendelevu wa mchakato wa mipango na utekelezaji. Kwa msingi wa ushiriki, wadau (Wizara za kisekta, Idara, Mawakala, sekta binafsi, vyama vya kiraia na washirika wa maendeleo) watakuwa sehemu kamili ya michakato ya upangaji mipango, ufuatiliaji na tathmini.

Katika vipindi vinavyolingana, ukusanyaji, uchanganuzi na uwekaji kumbukumbu wa data vitafanywa na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya kutumia taarifa pamoja, kujifunza na kuboresha. Mpango mkuu na mchakato wa ufuatiliaji wa umasikini ni sehemu kamili ya ufuatiliaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu.